# RARIEDA CLUSTER EXAMS-2025
## Kenya Certificate of Secondary Education

## 102/2 KISWAHILI (LUGHA) Karatasi ya 2

**Julai 2025-Muda: Saa $2^1/_2$**

---

**Jina**………………………..……………………**Nambari ya Mtahiniwa:**……………….**Sahihi**…………….

**Shule**………………..…………………………..**Tarehe**…………………………………….

---

**Maagizo**

(a) Andika jina na nambari yako ya mtihani katika nafasi ulizoachiwa hapo juu.
(b) Tia sahihi yako kisha uandike tarehe ya mtihani katika nafasi ulizoachiwa hapo juu.
(c) Jibu maswali **yote**.
(d) Majibu yote yaandikwe katika nafasi ulizoachiwa katika kijitabu hiki cha maswali.
(e) Majibu yote **lazima** yaandikwe kwa lugha ya Kiswahili.
(f) Usitoe ukurasa wowote kutoka kwenye kijitabu hiki.
**(g) Karatasi hii ina ukurasa 10 zilizopigwa chapa.**
**(h) Watahaniwa lazima wahakikishe kwamba kurasa zote za karatasi hii zimepigwa chapa sawsawa na kuwa maswali yote yamo.**

---

**Kwa Matumizi ya Mtahini Pekee**

| Swali | Upeo | Alama |
|---|---|---|
| 1.Ufahamu | 15 | |
| 2.Ufupisho | 15 | |
| 3. Lugha | 40 | |
| 4. Isimu Jamii | 10 | |
| JUMLA | 80 | |

**1. UFAHAMU** **(Alama 15)**

***Soma taarifa ifuatayo kisha ujibu maswali.***

Mwanamke wa kisasa anazaliwa na kukulia katika mazingira yaliyobadilika mno. Matazamio yake maishani ni tofauti na yale ya wanawake walioishi mapote mawili yaliyopita; wanawake makamu ya nyanyake na mamake mkuu.

Yeye alitarajiwa kuzaliwa, kukua, kuolewa, kuwa mke wa bwana, kumzalia watoto na daima dawamu kuwa ‘mwendani wa jikoni’ akawapikia watoto na bwanake chakula; na akitoka jikoni aelekee shambani kulima, kichakani kuchanja kuni, mtoni kufua nguo na kuteka maji ya kutumia nyumbani. Mwanamke wa kisasa huandamana na mwanamume. **Akanyagapo mume naye papo huutia wayo wake.**

Mwanamke wa kisasa huenda shule na kujifunza yote yafunzwayo huko. Hushindana na wanawake kwa wanaume na kuibuka mshindi si mara haba. Huibuka mshindi katika masomo ya lugha, Historia, Jiografia, Hesabu, Sayansi na mengineyo, sawa na mwanamume.

Mwanamke wa kisasa hutaka kufanya kazi za kibega, akazifanya. Akataka kuwa mwalimu, akawa.Akataka kuwa daktari, akafanikiwa. Almuradi, siku hizi mwanamke hufanya kazi yoyote ile afanyayo mwanamume. Kuna wanawake marubani wa ndege, masonara, waashi, wahandisi, madereva wa magari, mawakili mahakimu, mawaziri wakuu na hata marais wa nchi Hakuna kazi isiyofanywa na mwanamke siku hizi.

Mwanamke wa kisasa **hateswi akafyata ulimi.** Anapohiniwa yeye hupigania haki yake kwa dhati na hamasa. Katu hakubali ‘mahali pake’ katika jamii alipotengewa na wanaume wenye mawazo ya kihafidhina yaliyopitwa na wakati.

Siku hizi mwanamke huolewa tu wakati amepata kazi ya kumwezesha kujikimu maishani au pale anapokuwa na hakika kwamba biashara yake iwapo ni mfanyi biashara, imepiga hatua ya kutomrudisha **ukatani.**

Mwanamke wa kisasa haamuliwi katika jambo, lolote, bali hufanya maamuzi yake mwenyewe. Kwa upande mwingine, mwanamume wa ‘kisasa’, ambaye bado amefungwa pingu na taasubi za kiume, hapendezwi na mwanamke huyu. Huuma kidole akatamani ya kale, lakini wapi! Analazimika kumkubali mwanamke huyu kama

mshiriki sawa maishani, na kuishi naye, apende asipende. Shingo upande analazimika kukubali kwamba mabadiliko haya sio mithili ya kiwingu kipitacho, bali ni ya **aushi.**

**Maswali**

a) Mwanaume mhafidhina amemtengea mwanamke 'pahali pake'. Kwa kurejelea taarifa, eleza pahali alipotengewa mwanamke. ( Alama 6)

…………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………

………………………………………………………….........................

b) Fafanua jambo ambalo humsaidia mwanamke wa kisasa kufanya maamuzi ya kuingia kwenye ndoa. (Alama 2)

…………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………...........

c) Msemo 'mwendani wa jikoni' unadhihirisha hali gani ya mwanamke katika jamii? (Alama1)

…………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………..............

d) Mwandishi ana maana gani anaposema 'akanyagapo mume naye papo huutia wayo wake' (Alama 1)

…………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………..............

e) Fafanua athari zinazotokana na mabadiliko ya mwanamke wa kisasa katika jamii kulingana na mwandishi. (alama 3)

………………………………………………………………………………………………

………………………………………………………………………………………………

………………………………………………………………………………………………

………………………………………………………………………………………………

f) Eleza maana ya maneno yafuatayo kama yalivyotumika katika taarifa (alama 2)

i) ukatani

………………………………………………………………………………………

ii) aushi

………………………………………………………………………………………

## 2. MUHTASARI (ALAMA 15)

***Soma taarifa ifuatayo kisha ujibu maswali yatakayofuatia.***

Uvumbuzi wa nguvu za umeme umemfanya binadamu kurahisisha juhudi za kujipatia mahitaji yake.Jambo hili limeifanya dunia kuwa mahali pema zaidi pa kuishi. Kumekuwa na maendeleo,wala si kama enzi za mababu zetu zilizokuwa za giza. Kutokana na utafiti mwingi pamoja na majaribio mengi,njia chungu nzima za kutengeneza nguvu za umeme zimegunduliwa.Njiia hizo zimepanuliwa na kusambazwa kote na hata zimetia fora.Aina za nguvu ziinazotumiwa ni zile zinazotokana na maji, mvuke,jua,mafuta,upeo na hata samadi.

Umeme kutokana na maji ni maarufu sana ulimwenguni.Hii ndiyo njia ya kimsingi ya kutolea nguvu za umeme. Bwawa hujengwa kwenye mto kuhifadhi maji.Mifereji inayotoa maji haya bwawani huelekezwa kwenye magurudumu yanayoviringishwa na nguvu za maji hayo.Magurudumu haya nayo huzungusha nyuzi za shaba zilizowekwa sumaku na hivyo hutoa aina moja ya kawi . Isitoshe, kawi hii hubadilishwa ili kupata nguvu za umeme zinazohitajika.
Umeme unaopatikana husafirishwa kwa kutumia waya za shaba hadi kwenye vituo au sehemu zinazohitaji nguvu hizi. Nchini Kenya, vituo vinavyotoa stima – maji ni kama Kiambere, Wanjie,Turkwell, Masinga, Kamburu , Gitaru, na Kindaruma na vinginevyo.

Kutokana na milipuko ya volkeno pamoja na zilizala, njia nyingine ya kutengeneza nguvu za umeme imevumbuliwa. Njia hii inawezekana kwenye mahali palipo na chemchemi za maji moto kama huko Olkaria na mifereji ya chuma kuwekwa ili mvuke uelekezwe kwenye magurudumu yanayoviringishwa kasi na kutoa umeme.

Majenereta au vifanyiza vinavyotoa nguvu za umeme huonekana kila mahali nchini , hasa kwenye shule na hospitali . Majenereta haya hutumia mafuta ya aina ya taa, petroli au diseli. Kifanyiza kikiwashwa, mafuta haya huchomeka ndani ya injini ili kutoa nguvu za kuendesha mitambo ya kutengeneza umeme.

Stima – jua ni nguvu nyingine ambazo zimeanza kufanyiwa kampeni siku za hivi karibuni. Watu wamehimizwa kutumia stima – jua kwa sababu jua angani , hutoa mwanga unaombatana na joto kali , hasa katika sehemu za tropiki . Miale ya jua huangaza juu ya kioo kinachotengeneza nguvu hizi. Miale hii huelekezwa kwenye vidubwashadubwasha vilivyo chini ya kioo vinavyoibadilisha kuwa nguvu za umeme. Joto kutoka juani hutumika kuchemsha maji na kutolea nguvu za umeme nyumbani . Pia kuna umeme unaotokana na nguvu za tonoradi au nyukilia , lakini nguvu hizi hutumiwa na nchi kama sana,hasa zile zilizoendelea kama Urusi, Marekani, Uingereza, Ufaransa, Uchina, India, Israeli na Misri.

Samadi ya wanyama kama ngombe nayo hutumiwa kutengeneza aina moja ya kawi.Ikiwa katika hali ya majini , samadi hutiwa katika pipa maalum na kuongezewa maji. Matokeo yake ni gesi na joto linalotoa nguvu za umeme, ambavyo hupitia kwa kifaa kinachotiwa ndani ya pipa la samadi hiyo . Upepo na makaa ya mawe, pia hutumika kutengeneza nguvu za umeme katika sehemu zingine za ulimwengu.

**Maswali**

**a)** Fupisha aya mbili za mwanzo kwa maneno 50.

(alama 7. 1 mtiririko)

**Matayarisho**

…………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………

……………………………………………….........................................

…………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………

……………………………………………….............................................

**Nakala safi**

……………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………

………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………

…………………………………………

**b)** Eleza jinsi nguvu za umeme hupatikana. Tumia maneno kati ya 80-100.
(alama 8, 1 ya miririko)

**Matayarisho**

……………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………

**Nakala safi**

……………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………

**3. SARUFI NA MATUMIZI YA LUGHA** **(ALAMA 40)**

a) **Andika** neno lenye sifa zifuatazo; (alama 2)

nazali ya midomo, irabu ya wastani mbele tandazwa, nusu irabu ya midomo, irabu ya chini kati tandazwa

..........................................................................................................................

b) i **Andika** neno lenye silabi tatu za irabu. ( alama 1)

……………………………………………………………………………………

ii **Bainisha** muundo wa silabi kwenye neno: kwema ( alama 1)

……………………………………………………………………………………

c) **Eleza** maana zilizowakilishwa na viungo vidogo zaidi vya kisarufi katika;

amliliaye ( alama 3)

…………………………………………………………………………………………
…………………………………………………………………………………………
…………………………………………………………………………………………
…………………………………………………………………………………………
…………………………………………………………………………………………
……………………………………………………………........................

d) **Onyesha** miundo **minne** ya nomino katika ngeli ya U-ZI ( alama 2)

…………………………………………………………………………………………
…………………………………………………………………………………………
…………………………………………………………………………………………
……………………………………………………………………….................

e) **Andika** sentensi ifuatayo katika ukubwa. (alama2)

Ndama aliyenunuliwa sokoni ni wa mwalimu.

…………………………………………………………………………………….

f) i **Jaza** pengo (alama 2)

Robota ni kwa pamba,…………………….ni kwa askari na …………………..ni kwa nzige.

ii **Ainisha** vivumishi katika sentensi ifuatayo ( alama 2)

Mwalimu aliyeondoka jana atatuletea vitabu vizuri.

…………………………………………………………………………………………
……………………………………………………………………………….

iii **Tunga** sentensi mbili kubainisha dhima zifuatazo za kirai kihusishi . (alama 2)

kiwakilishi

…………………………………………………………………………………….

Kielezi

……………………………………………………………………………………

g) **Tambua** hali na nyakati katika sentensi zifuatazo. ( alama 2)

i) Sonara angali anafua dhahabu.

…………………………………………………………………………………………….

ii) Mtoto hajala chochote.

…………………………………………………………………………………………….

h) **Nyambua** vitenzi vifuatavyo katika kauli zilizo mabanoni. ( Alama 2)

pea …………… (tendeana)

funga …………… (tendama)

i) **Changanua** kwa mstari. (alama 4)

Mpenzi wake alimpenda kwa dhati lakini hakumheshimu sana.

………………………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………

j) **Eleza** maana **mbili** za sentensi ifuatayo; ( alama 2)

Baba mtoto amefika.

………………………………………………………………………………………………

………………………………………………………………………………………………

………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………..

k) **Unda** vitenzi kutokana na nomino zifuatazo (alama 2)

ufisadi ………………………………………………………………………………..

mapenzi ……………………………………………………………………………….

l) **Eleza** dhima za vishazi vilivyopigiwa mstari katika sentensi zifuatazo. (alama 2)

Vijana <u>waliopewa pesa</u> wanamsifu sana.

…………………………………………………………………………………

Nyanya alitaka tutambe <u>alivyotufundisha juzi</u>.

……………………………………………………………………………..

m) **Unganisha** sentensi zifuatazo ukianza kwa yambwa tendewa. (alama 2)

Vijana walisafisha soko. Soko ni la wanakijiji. Vijana walitumia fagio.

……………………………………………………………………………...

n) **Tunga** sentensi sahihi kubainisha matumizi yafuatayo ya -ki- ( alama 2)

Kielezi

……………………………………………………………………………...

Mazoea

……………………………………………………………………………

o) **Andika** katika usemi wa taarifa. ( Alama 3)

"Methali hii ninayokupigia ni ya tangu jadi wala si ya kuzua", Shafii alisisitiza.

………………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………

p) **Andika** kinyume cha sentensi ifuatayo (alama 1)

Mwanafunzi aliyesimama mbele ya gwaride amesifiwa na mwalimu.

………………………………………………………………………...

q) Timu yenye uzoefu katika kandanda ikishinda ile isiyo na uzoefu kwenye mchuano, je, ni methali gani huweza kutumika katika mazingira haya? (Alama 1)

………………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………

**4. ISIMUJAMII (ALAMA 10)**

*Watu nguyaz vipi? Leo hakuna wera bana. Msoto utatuua. Kwani hii gava ya hustler vipi? Haina form?*

*Itabidi tujikaze jo! Sir Godi ako na sisi.*

*Tuingie internet lazima kuna maadvert ziko. Huenda tukaangukia something.*

*(kutoka Nishati ya Sarufi na Isimujamii)*

a) Tambua sajili ya mazungumzo haya (alama 2)

.............................................................................................................................

.............................................................................................................................

.....................................................................................................................

b) Eleza sifa zingine tatu za sajili hii. ( alama 3)

………………………………………………………………………………………

………………………………………………………………………………………

………………………………………………………………………………………

………………………………………………………………………………………

………………………………………………………………………………………

………………………………………………………………………………………

………………………………………………………………………………………

c) Fafanua sababu tano zinazowafanya wahusika kutumia lugha kwa jinsi hii. (alama 5)

………………………………………………………………………………………

………………………………………………………………………………………

………………………………………………………………………………………

………………………………………………………………………………..............

.............................................................................................................................

**HUU NDIO UKURASA WA MWISHO ULIOPIGWA CHAPA**